

**KYELA COOPERATIVE UNION LIMITED**

**REG:AFF-MBY-KYC-DC-2022-2**



**TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI WA HUDUMA YA  
UTUNZAJI NA UENDESHAJI WA GHALA LA UFUTA YA  
KYECU LTD.**

**ZABUNI NA.1: GHALA LA UFUTA LILILOPO KYELA  
MJINI.**

**KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 .**

**TAREHE YA TANGAZO: 10 MAY, 2026**

## TANGAZO LA ZABUNI

Mwenyekiti wa bodi ya KYECU LTD anawatangazia wananchi wote wa Tanzania kuwa KYECU LTD inahitaji mtoa huduma kwa kazi ya utunzaji na uendeshaji wa ghala La Ufuta kwa msimu kwa mwaka 2026/2027.

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI
KYC/HDM/2026/2027/01-02	<p><b>ZABUNI YA HUDUMA YA UTUNZAJI NA UENDESHAJI WA GHALA LA UFUTA.</b></p> <p><b>ZABUNI(LOT) NA.1: GHALA LA UFUTA LILILOPO KYELA MJINI.</b></p> <p><b>UFUTA HUSIKA UTAKUWA UNATOKA KATIKA VYAMA VYA MSINGI (AMCOS) KWENDA KWENYE GHALA KUU LA KYECU LTD.</b></p>


## MASHARTI YA MWOMBAJI.

1. Mwombaji lazima awe Mtanzania.
2. Mwombaji awe na kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania (Ambatanisha cheti cha usajili wa kampuni);
3. Mwombaji awe na hati hai ya kuthibitisha ulipaji kodi (TAX CLEARANCE);
4. Mwombaji lazima awe na leseni ya biashara iliyo hai;
5. Mwombaji awe na Cheti cha usajili wa utunzaji wa maghala kutoka Bodi ya stakabadhi ya Maghala (WRRB).
6. Mwombaji lazima aambatanishe namba ya utambulisho ya mlipa kodi (TIN);
7. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha na athibitisha kwa kuambatanisha taarifa za benki (**Bank statement**) ya Miezi kumi na mbili (12), iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni na iwe imegongwa mhuri wa benki husika.

8. Mwombaji aambatanishe 'Power of Attorney' inayosimama na kuongelea zabuni husika.
9. Ada ya maombi ya zabuni ni Tsh 200,000/= (Laki mbili), Kiasi hicho kitalipwa kupitia akaunti ya chama **No.60903500112** jina la akaunti Kyela Cooperative Union Ltd ( Benki ya NMB ) na kukatiwa stakabadhi ya malipo ambayo itaambatanishwa katika barua ya maombi na fedha hizo hazitarudishwa.
10. Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema zabuni anayoomba na aambatanishe uthibitisho wa uwepo wa vifaa hivyo,kama vile hali ya umiliki(risiti na picha ya vifaa hivyo).
11. Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindani wa kitaifa (National competitive Tendering) uliyoainishwa kwenye Mwongozo na Sera ya Ununuzi na Ugavi wa Vyama vya Ushirika.
12. **Masharti ya nyongeza kwa mwombaji:-**
  - i. Mwombaji awe na vifaa sahihi kwa ajili ya kazi husika kama vile Vipima Unyevu, Paleti, Mizani ya Kidigitali, vifaa vya kuchukulia sampuli za Ufuta (Sample drawer),Kompyuta, Printa na viwe ni mali yake halali.
  - ii. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha kwa ajili ya kulipa wafanyakazi wake kwa wakati.
  - iii. Mwombaji aweke kiasi atakacholipa kwa kazi aliyoomba.
  - iv. Mwombaji atatumia ghala na ofisi zilizo katika eneo la ghala tu.
13. Kitabu cha zabuni na maelezo mengine yatapatikana ofisi ya Meneja Mkuu wa **KYECU LTD, S.L.P 415, KYELA** Kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri (Jumatatu hadi Ijumaa) isipokuwa siku za sikukuu.
14. Maombi yazingatie mahitaji na kuambatanisha viambatanishi kama vilivyoainishwa katika Tangazo la Zabuni na Kitabu cha Zabuni na kutumwa kwa **MENEJA MKUU KYECU LTD, S.L.P 415, KYELA.**
15. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (Original) moja(1) na nakala (Copy) moja (1) na zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri.
16. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya **E-MAIL, FAX,TELEFAX na TELEGRAFIC SYSTEM** hayatapokelewa.
17. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **18/05/2026 saa 4:00** asubuhi na kufunguliwa tarehe **18/05/2026 saa 4:30** asubuhi katika ofisi za

**KYECU LTD.** Waombaji mnakaribishwa kushiriki katika ufunguzi wa zabuni kwa gharama zenu.

18. Zabuni ifungwe kwa lakiri na iandikwe juu ya bahasha namba ya zabuni inayoomba.
19. Zabuni itakayochelewa kuwasilishwa, na isiyofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni kwa hali yoyote haitakubaliwa kwa Tathimini.
20. Maombi yote yawekwe kwenye sanduku la zabuni katika ofisi za Chama kikuu cha Ushirika Kyela (KYECU LTD).



**AMANI JOSEPHAT HANKUNGWE**  
**MENEJA MKUU**  
**KYECU LTD**  
**KYELA**

